



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI



Kumb. Na. HA.80/118/01/17

27 Oktoba, 2023.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji anapenda kuwatangazia Watanzania wenyе sifa kuomba nafasi za kazi ya Dereva daraja la II kwa sifa zifuatazo:-

1.Dereva daraja la II – Nafasi mbili (2).

1:1 Kazi za Kufanya.

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa gari
- Kufanya kazi nyingine kadri atavyoelekezwa na Msimamizi wake.

2.2 Sifa za Mwombaji.

- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne.
- Awe na leseni ya daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari(Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Mafunzo ya Ufundu Stadi(VETA) au Chuo Kingine kinachotambuliwa na Serikali.Waombaji wenyе cheti cha Majaribio ya Ufundu Daraja la II watafikiriwa kwanza.

2.3 Ngazi ya Mshahara.
Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikali yaani TGS B/1 kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA

12. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania
13. Waombaji wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45
14. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za wadhamini watatu.
15. Waombaji wote waambatishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) au waandike namba za NIDA kwenye CV na barua za maombi
16. Waombaji wote waambatishe na Nakala za Vyeti vya Elimu na Taaluma kwa mujibu wa sifa ya kila kada
17. Waombaji waambatishe na nakala za cheti cha kuzaliwa
18. Maombi yaambatishwe na picha mbili za rangi (pass port size) zilizopigwa hivi karibuni
19. Result slip, statement of Result, testimonial hazitakubaliwa
20. Waombaji ambao ni watumishi wa Umma wapitishe maombi yao kwa waajiri wao wa sasa
21. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificate) kutoka baraza la mitihani la Tanzania
22. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 28,
UTETE/RUFIFI

Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya mkono hayatapokelewa.
Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 09.11.2023 saa 9:30 Alasiri.

Imetolewa na:



Dk. Hamis Abdallah .

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
RUFIFI.**

Nakala:

- Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.
- Mbao zote za Matangazo